

"Ulul Amr" Ni Nani?

Allah Anasema katika Kitabu chake kitukufu:

"Enyi mlioamini Mtiini Allah, na mtiini Rasuli (Wake Muhammad) na Wale waliopewa mamlaka kutoka miongoni mwenu, (Qur'ani, 4:59)

Aya hii inawawajibisha Waislamu aina mbili za utii. Kwanza, kumtii Allah; Pili kumtii Rasuli. Hii ina maana kwamba ni lazima "Ulul Amr" wawe na cheo kama kile cha Rasuli; au sivyo Allah asingetuamrisha kuwatii wao na kule kumtii Rasuli, katika Aya hii.

Kabla hatujaamua ni nani hao "Ulul Amr", ingetusaia sana kama tungeitazama ile amri ya kumtii Rasuli [s], ili tuone jinsi amri hii inavyozunguka na kuenea kote-kote, na jinsi mamlaka ya Rasuli wa Allah [swt] ilivyo kuu.

Allah Anasema katika Qur'ani Tukufu:

"Na Hatukumtuma Rasuli yeyote ila atiiwe kwa idhini ya Allah..." (Qur'ani 4:64)

Ilibidi Manabii na Marasuli watiwe na kufuatwa, sio kwamba hao wafuasi walitegemewa kukicheki kila kitendo cha Nabii na kuamua kipi kitiwe na kipi kisitiwe. Hii inathibitisha wazi wazi kwamba, Manabii na Marasuli walikuwa Ma'asumiin (Wasiotenda madhambi wala kukosea); na lau isingekuwa hivyo, Allah Asingewamrisha watu kuwatii Marasuli bila ya masharti yoyote.

Ziko Aya nyingi za Qur'ani Tukufu ambazo ndani yao Allah Anatuamrisha kumtii Rasuli, Akisema:

"Enyi mlioamini: Mtiini Allah na mtiini Rasuli....."

Tena Allah Anasema:

"Na mwenye kumtii Allah na Rasuli....." (Qur'ani 4:69)

Katika Sura hiyo hiyo inathibitishwa kwamba:

"Mwenye kumtii Rasuli amemtii Allah....."

Katika aya zote hizi za Qur'ani Tukufu na nyinginezo nyingi, utii kwa Allah umefanywa kuwa sawa na utii kwa Rasuli. Uthibitisho huu usingewezekana kama Manabii wasingekuwa Ma'asumiin na Watakatifu.

Sasa hebu ongezea aya hii ifuatayo katika aya tulizozitaja hapo juu:

"...Wala usimtii miongoni mwao mwenye dhambi." (Qur'ani 76:24)

Sasa picha imekamilika. Inabidi kuwatii Manabii. Watendao madhambi wasitiwe: Hivyo, uamuzi ni kwamba, Manabii si watenda madhambi. Kwa usemi mwingine ni kwamba, Manabii ni Ma'asumiin (Watakatifu) na Wasiotenda Madhambi.

Hebu fikiria ni hali gani ambayo ingetokea kama Nabii yeyote yule angewasihi wafuasi wake wafanye kosa fulani au dhambi. Kwa vyo vyote vile hawa wafuasi waovu wangelaaniwa na kuipata ghadhabu ya Allah. Kama wakimtii Nabii yule na kuitenda ile dhambi wangukuwa wameihalifu amri ya Allah na hivyo wangufedheheshwa. Na kama kwa upande mwingine, wakimwasi yule Nabii, vivyo wangukuwa wameiasi amri ya Allah tuliyoitaja hapo juu yenye kuhusu kumtii Nabii. Hivyo yaonekana kwamba Nabii asiye Ma'asuum asingeweza kuwaletea watu wake cho chote kile ila fedheha na laana tu.

Tukimtazama hasa Mtukufu Mtume wetu [s] tunaona kwamba Allah Ametuamrisha Akisema:

"...Na anachokupeni Rasuli basi kipokeeni; na anachokukatazeni jiepusheni nacho...." (Qur'ani, 59:7)

Hii ina maana kwamba, kuruhusiwa au kukatazwa na Mtukufu Mtume [s] kila mara kulikuwa kukitegemeana na Mapenzi ya Allah na kila mara Alikupenda. Hii inathibitisha kwamba Mtukufu Mtume [s] alikuwa Ma'asum. Hakuna mtu awezaye kuwa na uhakika kabisa kabisa juu ya amri azitoazo mtu asiye Ma'asum.

Iko aya nyingine isemeyo:

"Sema (ewe Rasuli wetu Muhammad); Kama ninyi mwampenda Allah, basi nifuateni (na) Allah Atakupendeni na Atakughofirieni madhambi yenu...." (Quran, 3:31)

Katika aya hii, kumpenda Allah kumetegemezwa na kumfuata Mtukufu Mtume [s]. Pande zote mbili za mapenzi zimejumlishwa ndani yake. Kama unampenda Allah basi mfuate Mtume [s] kama ukimfuata Mtume [s] Allah atakupenda. Je, hii haionyeshi kwamba Mtukufu Mtume [s] alikuwa katoharika kabisa na kila aina ya dosari?

Si matendo yake tu, bali hata maneno yake yalikuwa ni amri ya Allah. Allah Anasema katika Qur'ani Tukufu:

"Wala hasemi (huyu Rasuli Wetu Muhammed) kwa matamanio yake. Sio hayo ila ni ufunuo uliofunuliwe kwake." (Qur'ani, 53:3-4)

Katika aya hizi tunaiona daraja ya hali ya juu sana ya Utakatifu awezayo kuifikiria mtu.

Vile vile ziko aya kadhaa katika Qur'ani Tukufu ambazo ndani yake maneno yafuatayo yametumiwa kwa ajili ya Mtukufu Mtume wetu [s].

"... Rasuli kutoka miongoni mwao, awesomee ishara zake na kuwatakasa na kuwafunza Kitabu na Hekima....." (Qur'ani, 62:2)

Vipi Nabii ataweza kuwatakasa watu kutokana na madhambi na dosari iwapo yeye mwenyewe si Mtakatifu. Vipi mtu ataweza kuwafundisha wenzie hekima ikiwa yeye mwenyewe hana hekima imwezeshayo kupambanua baina ya ukweli na uwongo – Au lililo baya zaidi, pale akosapo uwezo wa nia ya kujizuia kutenda uovu pale anapoufahamu – Kazi ya Mtukufu Mtume [s] ilikuwa kuwafundisha watu Kitabu cha Allah. Hii ina maana kwamba yeye Mtukufu Mtume [s] alizijua amri za Allah.

Ilikuwa kwamba awatakase na kuwafundisha hekima; hii ina maana kwamba yeye mwenyewe alikuwa ne hekima na tohara.

Uthibitisho wa ukamilifu wa tabia zake unapatikana katika Qur'ani Tukufu, katika aye isemayo:

"Na hakika (Wewe Rasuli Wetu Muhammad) une tabia njema adhimu" (Qur'ani, 68:4)

Mtu atendaye maovu hawezi kuistahili sifa hii. Aya zote hizi zaonyesha mambo mawili:

Jambo la Kwanza: Mamlaka ya Mtukufu Mtume [s] juu ya Waumini haina kikomo na ni yenye kuenea kote kote. Amri yoyote aitoayo, katika hali yoyote ile, mahali popote pale, na wakati wowote ule, ni wajibu kuitii bila ya swali lolote lile.

Jambo la Pili: Ni kwamba, yeye alipewa mamlaka kubwa sana kwa sababu ni "Ma'asum" (Mtakatifu) na katoharika kutokana na makosa, na madhambi. Isingekuwa hivyo, Allah Asingetuamrisha kumtii bila ya masharti yoyote yale.

Sasa katika aya hii (Qur'ani, 4:59), hawa "Ulul Amr" wamepewa mamlaka iliyo sawa kabisa na hii juu ya Waislamu, kwa sababu wote, "Rasuli" na hawa "Ulul Amr" wametajwa kwa pamoja, chini ya neno moja, Ati-'uu" (Mtiini) jambo ambalo laonyesha kwamba kuwatii "Ulul Amr" kuna maana ile ile ya kumtii Rasuli.

Hii yaonyesha kwamba "Ulul Amr" nao ni lazima wawe "Ma'asum" (Watakatifu), na waliotakasika kabisa kutokana na kila aina ya makosa, ne madhambi, au sivyo amri ya kuwatii wao isingeingwa na amri ya kumtii Rasuli [s].

Imamu wetu wa kwanza Amirul Mu'miniin Ali bin Abi Talib [a] alisema:

"Yeyote yule amwasiye Allah asitiwe; na hakika utii ni wa Allah na Rasuli Wake na wale waliopewa mamlaka. Hakika Allah ameamrisha kumtii Rasuli kwa sababu yu Ma'asum, aliyetoharika na ambaye katu hatawaamuru watu kumwasi Allah; na hakika Aameamrisha kuwatii wale waliopewe mamlaka kwa

sababu wao (nao) si watenda madhambi; wametoharika na hawawezi kuwaamuru watu kumwasi Allah."

(Kifungu hiki kimenukuliwa kutoka kitabu 'Ilalu Sharaye', kama kilivyonakiliwa katika Tafsiri Safi).

Kabla hatujaendeleo zaidi, inatlazimu tueleze kuwa Waislamu wengi (Masunni) huyatafsiri maneno haye "Ulul Amr" kuwa na maana ya 'Watawala kutoka miongoni mwenu, yaani watawala wa Kiislamu. Tafsiri hii haina msingi wowote wa kihaja. Haja yake imesimama katika msingi wa upotoshaji wa historia ya Kiislamu. Waislamu wengi wamekuwa vibaraka wa wafalme na watawala wakiutafsiri Uislamu na Qur'ani kwa kurudia ili kuwaridhisha watawala wa kila zama.

Ulikuwapo wakati ambao ufalme ulikuwa aina ya pekee ya utawala iliyotumika. Katika zama hizo wanachuoni wa Kiislamu walikuwa wakiwatukuza wafalme na milki zao kwa kusema kuwa "Mfalme ni kivuli cha Allah" (Kana kwamba Allah ana kivuli). Siku hizi demokrasi ndio mtindo wa serkali na wanachuoni wa Kisunni hawachoki kuthibitisha katika maandishi yao, vitabu vyao na matoleo yao kuwamsingi wa Utaratibu wa serkali ya Kiislamu ni demokrasi. Huendelea hata kuthubutu kusema kuwa demokrasi ilianzishwa na Uislamu, wakisahau kabisa Jamhuri za miji ya Uyunani (Ugriki) za zamani sana hata kabla ya Uislamu.

Katika nusu ya pili ya karne hii, ujamaa na ukomunisti vinazidi kuenea katika nchi zinazoendelea na wala sitashangaa kusikia kuwa wanachuoni wa Kiislamu wanajaribu kila wawezacho ili kuthibitisha kuwa Uislamu unafundisha na kujenga Ujamaa. Baadhi ya watu katika nchi ya Pakistani na mahali penginepo wamezua usemi usemao "Ujamaa wa Kiislamu." Maana hasa ya huu "Ujamaa wa Kiislamu", mimi sijui. Lakini mtu asishangae kuona kuwa katika muda wa miaka ishirini ijayo watu hawa hawa wataanza kudai kuwa Uislamu unafundisha Ukomunisti.

Mambo yote haya hubadilika ili kuudhihaki utawala wa Kiislamu.

Miaka michache iliyopita katika mkutano wa Waislamu uliofanyika katika nchi ya Kiafrika, ambao rais wa nchi hiyo alikuwa mgeni wa heshima, kiongozi wa Kiislamu alisema katika hotuba yake kuwa Uislamu unafundisha "Mtiini Allah, Mtiini Rasuli na watawala wenu".

Katika Jibu lake, rais huyo (ambaye aliheshimiwa ulimwenguni pote kuwa yu kiongozi mwenye hekima na ambaye alikuwa ni Mkristo wa Kanisa Katoliki), alisema kuwa alipendezewa sana na hekima iliyomo katika amri ya kumtii Allah na Rasuli wa Allah, lakini hakuweza kuelewa haja za amri ya kuwatii watawala wenu. Je, vipi iwapo mtawala huyo atekuwa mdhalimu na mwonevu? Je, Uislamu unaamrisha kumtii mtawala huyo kabisa kabisa bile ya kumpinga?

Hakika swali hili la kihakima linahitaji jibu la kihakima vile vile, wala haliwezi kutupiliwa mbali. Ukweli ni kuwa kiongozi yule wa kidini aliyesema vile, kasema kutokana na kuitafasiri vibaye Qur'ani. Historia ya Kiislamu imejaa majina ya watawala ambao udhalimu wao, uasherati wao na uonevu vimeiiharibu jina la Uislamu. Watawala kama hao kila mara wamekuwepo na bado wapo na watakuwepo hata pengine zaidi ya hao.

Ili kukupa mifano michache:

Yazidi bin Muawiyyah: Alikuwa Khalifa wa Uislamu. Lakini imani yake na tabia zake vilikuwaje? Yeye alikataa kabisa kumwamini Mtukufu Mtume [s]. Alionyesha wazi wazi imani yake katika Shairi lake lisemalo:

"Bani Hashim (Mtume [s] na Ahlul-Bait wake) walivumbua mbinu za kupatia milki. Kwa hakika hakukuwepo na habari zozote zitokazo kwa Mwenyezi Mungu wala Ufunuo wowote."

Yazid hakuamini siku ya Mwisho. Anasema:

"Enyi wapenzi wangu (msiamini kuwa mtakutana nami baada ya kufa kwangu maana) yale walivyokuambieni kuhusu kufufuliwa baada ya kufa, kwa ajili ya Hukumu ni uzushi uufanyao moyo uzisahau fahari (za ulimwengu huu wa kweli)."

Baada ya kuupata Ukhalifa, aliidhihaki Sala ya Kiislamu waziwazi; akaonyesha kutoiheshimu dini kwa kuwavisha mbwa na ngedere mavazi ya viongozi wa kidini. Kamari na kucheza na madubu vilikuwa michezo yake ya kawaida. Alitumia muda wake wote katika kunywa kila mahali bila ya kusita; hakuwa na heshima kwa mwanamke yeyote na hata 'mahramu' wake kame vile mama, umbu, shangazi, mama mdogo na binti. Hawa wote walikuwa sawa na wanawake wengine mbele yake.

Mauwaji ya watu wa Nyumba ya Mtume [s] aliyoyafanya yanajulikana sana. Ulimwengu unafahamu kabisa yale yaliyotokea huko Karbala na jinsi Imamu Husayn [a] na masahaba wake na ndugu zake (akiwemo mtoto mwenye umri wa miezi sita) na jinsi wote hawa walivyokufa kishahidi mnamo tarehe 10 ya Muharram (Mfunguo 4) mwaka 61 A.H. jinsi watukufu hao walivyowekwa na njaa na kiu tangu tarehe 7 hadi 10 ya mwezi huo; jinsi mahema yao yalivyochomwa na jinsi familia yake (wakiwemo wanawake, watoto na mwanawe aliyekuwa mgonjwa sana) walivyofanywa mateka na kupelekwa Kufa na baadaye kupelekwa Demeshki; jinsi walivyotiwa jela kwa mwaka mzima kabla ya kufunguliwa. Mambo haya yanajulikana sana na hayana ulazima wa kuelezwa kwa kirefu hapa.

Baada ya mauwaji ya Karbala, Yazid alituma jeshi lake kwenda Madina. Mji huo Mtakatifu wa Mtume [s] ulitekwa nyara. Wasichana bikira mia tatu; achilia mbali wanawake wengine, walinajisiwa. "Quarii" (Wasomaji wa Tajwiidi) wa Qur'ani mia tatu na masahaba mia saba wa Mtume [s] waliuwawa kikatili. Msikiti Mtakatifu wa Mtume [s] ulifungwa kwa muda wa siku kadhaa; jeshi la Yazid liliutumia msikiti huo kama banda la farasi wao. Mbwa waliingia msikitini humo na Mimbari ya Mtume [s] ilinajisiwa na wanyama hao. Mwisho amiri jeshi wa Yazid aliwalazimisha watu wa Madina kumkubali Yazid kwa kuapa kwa meneno haya:

"Sisi tu watumwa wa Yazid; ni juu yake kutupa uhuru au kutuuza katika soko la watumwa."

Wale waliotaka kuapa kiapo cha utii kwa Yazid chini ya masharti ya kuwa 'Yazid afuate Qur'ani na Hadithi za Mtume [s] waliuawa.

Baada ya hapo, kwa amri ya Yazid jeshi lilikwenda Makkah. Mji huo wa Allah ulio mtakatifu kuliko yote duniani, ulizingirwa. Jeshi hilo halikuweza kuingia mjini humo, hivyo ikabidi askari watumie teo (fumbewe au kombeo–silaha ya kivita ya zamani sana iliyotumika kwa kutupia mawe mazito katika sehemu zilizo mbali).

Kwa kutumia teo walitupa mawe na vijinga vya moto katika Kaaba. 'Kiswa' (yaani nguo iifunikayo Kaaba ikaungua na sehemu ya jengo hilo takatifu ikaanguka.

Na sisi tunategemewa kuamini kuwa Yazid alikuwa mmoja wa 'Ulul Amr' ambae kumtii kulikuwa wajibu kama kule kwa Mtume [s].

Source URL:

<https://www.al-islam.org/ulul-amr-ni-nani-sayyid-saeed-akhtar-rizvi/ulul-amr-ni-nani#comment-0>